# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

***OFISI YA RAIS***
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA

*Barua zote ziandikwe kwa:*
*Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,*
*Simu Na 023 2402738,*
MKURANGA,
*Fax Na 023 402706*
*Unapojibu tafadhali taja:*

S.L.P. 10,

PWANI.

**Kumb. Na. LD/MK/6272/13** **8/12/2021**

Mkurugenzi Mkuu,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P.938,
**Dar es salaam**

**YAH: KUITAMBULISHA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA MANISH HOME NEEDS INDUSTRIES LIMITED KUMILIKI KIWANJA NA.1 KITALU 'DD' VIKINDU MADAFU, WILAYA YA MKURANGA**

Rejea mada tajwa hapo juu.

Ninakujulisha kwamba, kiwanja tajwa hapo juu kimetokana na upimaji wa eneo lililonunuliwa na kampuni ya **Manish Home Needs Investment Industries** na kisha kupimwa kwa kuzingatia Ramani ya Mipango Miji Na.19/MKR/519/072018 kwa matumizi ya Kiwanda

**Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999, fungu la 19-20 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na.26 ya mwaka 1997, aidha kwa kuzingatia fungu la 12 na 179 Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 na Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, kanuni za Ardhi za 2001, kanuni ya 9C(v), kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania.**

Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi kwako ili iweze kupatiwa Certificate of Incentive yenye kuonyesha namba ya kiwanja uwekezaji utakapofanyika ili kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya kuandaa **Designation for Investment-Land form Na.1** ili kiwanja hiki kigawiwe katika **kamati ya Ugawaji wa Ardhi Taifa na kisha** kitangazwe kuwa cha Uwekezaji katika Gazeti la Serikali.

Nawasilisha kwako kwa hatua zaidi, nimeambatanisha nyaraka muhimu kwa urahisi wa rejea **(Hati ya ununuzi wa eneo, Usajili wa Kampuni, Ramani ya Mipango Miji na Upimaji, MoU and Article of Association, mikataba ya kupatikana kwa Ardhi na nyaraka zote muhimu).**

Nawasilisha kwako kwa hatua zako muhimu.

Chagiye R.M
Kny.Mkurugenzi Mtendaji (W),
**Mkuranga.**

**Nakala:** Mkurugenzi Mtendaji (W)
**Mkuranga** -Kwa taarifa

Manish Home Needs Industries Limited
S.L.P. 1120
**Dar es salaam** -Fuatilia nyaraka husika TIC